JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

TANGAZO

KUFUNGULIWA KWA UVUVI WA KAMBAMITI KWA MSIMU WA MWAKA, 2027

(Chini ya Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uvuvi, Sura 279)

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inalo jukumu la kisheria la kusimamia, kulinda, na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini na kuhakikisha rasilimali hizi zinanufaisha jamii na Taifa kwa ujumla. Ili kufanikisha malengo yanayokusudiwa Wizara ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi zilizopo na kutoa miongozo mbalimbali ya kusimamia uvuvi endelevu wa samaki aina ya Kambamiti kwa lengo mahususi kudhibiti upotevu na upungufu wa rasilimali hizi muhimu za uvuvi.

2. Kama mnavyofahamu uvuvi wa samaki aina ya Kambamiti hufanyika nchini katika kanda ya Kaskazini na Kusini. Kwa kuzingatia majukumu niliyokasimishwa kwa mujibu wa sheria naelekeza kwa msimu wa mwaka 2027 maombi ya leseni na uvuvi huu na msimu wa uvuvi utafanyika kama ifuatavyo:-

i. Kanda ya kaskazini inahusisha maeneo ya Dar es Salaam, Tanga, Bagamoyo – Saadani. Kwa kanda hii uvuvi utafanyika kuanzia tarehe 1 Machi hadi tarehe 30 Septemba, 2027

ii. Kanda ya kusini inahusisha maeneo ya Kisiju, Rufiji - delta, Jaja/Kilwa, Lindi na Mtwara. Kwa kanda hii uvuvi utafanyika kuanzia tarehe 1 Aprili hadi 31 Agosti, 2027

iii. Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti unaofanywa na wavuvi wakubwa, maombi yatumwe kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

iv. Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti unaofanywa na wavuvi wadogo maombi yatumwe Halmashauri kulingana na eneo ambalo muombaji atafanya uvuvi. Maombi hayo yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika.

3. Kwa tangazo hili naelekeza kila kampuni au mwananchi mwenye nia ya kufanya uvuvi wa Kambamiti kwa msimu wa mwaka 2027 atume maombi ndani ya **siku kumi na nne (14)** kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha, waombaji wanapaswa kuzingatia Sheria ya Uvuvi [Sura 279], Kanuni ya Uvuvi za Mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2020. Kwa maelezo zaidi waombaji wanaombwa kutembelea Ofisi za Wizara Kanda ya Dar es Salaam na Pwani na tovuti ya wizara *(www.mifugo.uvuvi.go.tz)*

4. Tangazo hili limetolewa kwa mujibu wa Sheria. hivyo, ukiukwaji wa waraka huu ni kosa na hatua za kisheria zitachukuliwa.

Agnes K. Meena
KATIBU MKUU